BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA KAMATI YA BAJETI KUHUSU MAJUMUISHO YA MJADALA WA BAJETI ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia uhai na uzima tukaweza kukutana tena leo hii katika Baraza lako tukufu ili kutekeleza majukumu yetu ya kuwawakilisha wananchi wa Zanzibar ya kujadili na kupitisha Bajeti za Wizara na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kuniruhusu kwa niaba ya Kamati ya Bajeti kusoma Hotuba hii ya Kamati kuhusu Majumuisho ya Mjadala wa Bajeti kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Katika Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Baraza la Kumi la Wawakilishi, Waheshimiwa Wajumbe walijadili na kupitisha bajeti za Wizara zote kumi na nane (18). Napenda kuchukua fursa hii kuwakumbusha Mawaziri na Serikali kwa ujumla kwamba, michango na hoja mbali mbali ambazo Wajumbe wamezitoa hazikuwa na dhamira ya kuikwamisha Serikali wala kuikandamiza, bali ilikuwa na lengo la kuikosoa na kuishauri Serikali ili kuzirekebisha na hatimae kuzifanya bajeti za Wizara zetu ziwe bora zaidi. Aidha, nawanasihi Mawaziri wote kwamba yale muliyoyaahidi kuyachukua na kuyafanyia kazi, mutekeleze ahadi hizo kwa vitendo ili tija na ufanisi upatikane katika utekelezaji wa bajeti zetu. Jambo hili litalipa heshima kubwa Baraza na Serikali kwani Wajumbe wametumia muda mwingi kujadili na kutoa ushauri wao.

Mheshimiwa Spika, Shukurani maalum naomba nizipeleke kwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti inayoundwa na Wajumbe mahiri ambao nakiri kwamba
michango, maoni na ushauri wao umewezesha kufanikisha kazi za Kamati ya Bajeti

kutekelezeka kwa ufanisi mkubwa. Ili kuzipa nguvu shukurani zangu kwao, naomba uniruhusu niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo:

1. Mhe. Abdulla Hussein Kombo — Mwenyekiti
2. Mhe. Asha Abdalla Mussa — Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed — Mjumbe
4. Mhe. Issa Haji Ussi Gavu — Mjumbe
5. Mhe. Miraji Khamis Mussa — Mjumbe
6. Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad — Mjumbe

Aidha, napenda pia kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa ushirikiano wake na uratibu mzuri wa shughuli za Kamati. Sekreterieti hiyo inaundwa na makatibu wanne (4) ambao ni:

1. Ndg. Abass Vuai Moh'd — Katibu
2. Ndg. Asha Said Mohamed — Katibu
3. Ndg. Husna Rajab Othman — Katibu
4. Ndg. Shaib Fadhil Shaib — Katibu

Mheshimiwa Spika, Msingi wa hotuba hii ni matakwa ya Kanuni ya 101(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2020 ambayo inaelekeza Serikali kwa kushirikiana na Kamati ya Bajeti kufanya majumuisho kwa kuzingatia hoja zilizoibuka wakati wa mjadala wa Bajeti za Wizara.

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza matakwa ya Kanuni hiyo, Kamati yangu ilifanya vikao na Wizara mbali mbali na kujadiliana kuhusu Hoja za kibajeti zilizoibuka hususan zile hoja ambazo zilihitaji kupatiwa ufafanuzi wa ziada ambao ulikosekana au haukuridhisha wakati wa kupitisha mafungu ili majibu yake yawasilishwe Barazani. Hivyo, hotuba hii ni matokeo ya majibu hayo ya Serikali pamoja na maoni na ushauri wa Kamati.

UFAFANUZI WA HOJA ZILIZOJADILIWA WAKATI WA KIKAO CHA MAJUMUISHO BAINA YA SERIKALI NA KAMATI YA BAJETI

Mheshimiwa Spika, Katika kikao cha majumuisho baina ya Kamati na Wizara

ambazo baadhi ya hoja zake hazikupatiwa ufafanuzi wa kutosha wakati wa kupitisha bajeti zake, kulikuwa na jumla ya hoja tano (5) zilizojadiliwa kutoka katika Wizara zifuatavyo:

i. Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda
ii. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
iii. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi
iv. Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi
v. Afisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

Mheshimiwa Spika, Kwa lengo la kurahisisha ufafanuzi wa hoja zilizofanyiwa kazi na Kamati ya Bajeti, zimewekwa katika mfumo wa Jadweli ambalo limegawika Sehemu Tatu; **Sehemu ya Kwanza** inahusu Hoja Zilizoibuka, **Sehemu ya Pili** inahusu Majibu ya Wizara na **Sehemu ya Tatu** ni Maoni na Ushauri wa Kamati.

JADWELI: HOJA ZILIZOIBUKA

WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA			
SNo.	HOJA ZILIZOIBUKA	MAJIBU YA WIZARA	MAONI YA KAMATI
1.	Katika makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2023/2024 hakuna taarifa ya mapato yatokanayo na Shirika la Biashara Zanzibar (ZSTC). Kamati inaomba kupatiwa ufafanuzi wa mapato hayo. Aidha, kwa kuwa mapato na matumizi haya yanapitishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika. Kamati inahitaji ufafanuzi wa namna makadirio ya mapato na matumizi ya Shirika yalipitishwa ngazi ya Shirika kwani hadi kufikia mwezi Aprili Shirika halikuwa na Bodi ya Wakurugenzi.	Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) kwa mwaka wa fedha 2023/2024 limepanga kutumia jumla ya TZS 96.7 bilioni. Kwa upande wa Mapato Shirika linatarajia kukusanya jumla ya TZS 97.4 bilioni kutoka vyanzo vyake mbalimbali. Mapato na Matumizi ya Shirikia yanatapitishwa na Bodi ya Wakurugenzi, ni kweli bodi imemaliza muda wake na tunatarajia muda si mrefu tutapata Bodi mpya. Hivyo kwa kipindi hiki majukumu yake yanapita kwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda.	Licha ya bajeti kupitishwa kwa utaratibu wa kupitia kwa Waziri, Kamati inaishauri Serikali kuwa na usimamizi wa karibu wa utendaji wa bodi pamoja na kufahamu muda wa kumaliza kwake ili ziweze kuundwa upya pale zinapomaliza muda wake. Hatua hii itasaidia kuepusha uvunjaji wa sheria zinazounda Shirika au Taasisi husika ambazo zinaelekeza bajeti kupitia katika Bodi za Wakurugenzi kabla kufikishwa katika ngazi ya Wizara.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO			
SNo.	HOJA ZILIZOIBUKA	MAJIBU YA WIZARA	MAONI YA KAMATI
1.	Katika makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2023/2024, kwenye viashiria kuna wazee 31,000 watakaopatiwa Pencheni Jamii lakini katika kifungu cha bajeti hamna fedha iliyopangwa. Katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri alieleza kwamba fedha hizo zipo katika Afisi ya Rais - Fedha na Mipango. Kamati inaomba ufafanuzi ni kwa namna gani itaweza kufanya shughuli za uratibu bila ya bajeti yoyote. Kamati inaomba ufafanuzi pia ni utaratibu gani umetumika kwa fedha za Wizara ya Maenedeleo ya Jamii kutumiwa na Afisi ya Rais - Fedha na Mipango.	Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeweka fungu lisilo na fedha kwenye Uratibu wa Pencheni Jamii ndani ya Bajeti iliyowasilishwa licha ya kwenye viashiria kuonyesha kuna wazee 31,000 watakaopatiwa Pencheni Jamii kwa sababu Serikali imefikia maamuzi ya kuhamisha fedha zote za Pencheni Jamii kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii na kuzipeleka Afisi ya Rais - Fedha na Mipango.	Kwa kuzingatia kuwa fedha zote za Pencheni ya Jamii zitaingizwa katika Fungu la Afisi ya Rais - Fedha na Mipango na kwa kuwa uratibu utafanywa kwa mashirikiano baina ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Afisi ya Rais - Fedha na Mipango, Kamati inasisitiza kuwepo kwa uwazi katika kufanya uratibu huo ili kuhakikisha kunakuwepo na utaratibu mzuri wa upatikanaji wa fedha hizi ili utekelezaji wake uweze kufanyika kwa wakati. Kamati pia inashauri kuangaliwa vyema Kifungu cha 31 cha Sheria ya Masuala ya Wazee ya 2020 ili mpango huu usije ukaratibiwa kinyume na Sheria hiyo.

WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI			
SNo.	HOJA ZILIZOIBUKA	MAJIBU YA WIZARA	MAONI YA KAMATI
1.	Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Shirika la Meli limepanga kuanza ujenzi wa boti mbili za mwendo kasi zitakazokuwa na uwezo wa kusafirisha abiria 650 kila moja. Boti hizi zitafanya kazi ya usafirishaji abiria baina ya Unguja, Pemba, Tanga na Dar es Salaam. Kwa kuwa, kwa mujibu wa Kifungu cha 105 (1)(f) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 ambacho kinaeleza kwamba taarifa za Mashirika ya Umma zinapaswa kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi, hivyo Kamati inahitaji kupatiwa taarifa za makadirio ya mradi wa ujenzi wa boti mbili za mwendo kasi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.	Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Shirika la Meli imepanga kujenga boti mbili za mwendo kasi zitakozofanya safari baina Pemba, Tanga, Dar es Salaam na Unguja. Boti hizi kila moja inakadiriwa kugharimu Dola za Kimarekani milioni 11. Hivyo, kwa boti mbili zinakadiriwa kugharimu Dola za Kimarekani Milioni 22. Fedha zitakazotumika kwa ajili ya ujenzi wa boti hizo ni mkopo utakaokopwa na Shirika la Meli chini ya Udhamini wa Afisi ya Rais - Fedha na Mipango.	Kamati imekubaliana na majibu yaliyotolewa katika hoja hii kuhusiana na makisio ya fedha za mradi wa ujenzi wa boti. Aidha, kwa kuwa, fedha hizo zitakopwa na Shirika la Meli, Kamati inalitaka Shirika kuwa na mipango madhubuti ya matumizi ya fedha hizo katika utekelezaji wa mradi uliokusudiwa pamoja na kuweka mpango maalum wa namna ya kurudisha fedha hizo za mkopo kwa wakati ili kuepusha deni kuongezeka kutokana na kuongezeka kwa riba ya mkopo huo kutakakotokana na kuchelewa kulipwa kwa deni.

WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI			
SNo.	HOJA ZILIZOIBUKA	MAJIBU YA WIZARA	MAONI YA KAMATI
1.	Kwa kuwa makadirio ya mapato na matumizi ya Bodi ya Usajili ya Wakandarasi Zanzibar na Wakala wa Majengo yanapitishwa na Bodi za Wakurugenzi za taasisi hizo, na kwa kuwa taasisi hizo hazikuwa na Bodi za Wakurugenzi, Kamati inaomba ufafanuzi wa taratibu zilizotumika kupitishwa makadirio ya mapato na matumizi ya taasisi hizi katika ngazi ya taasisi husika kabla kuletwa Barazani kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi?	Kwa kuwa Bodi za Wakurugenzi za Bodi ya Usajili ya Wakandarasi Zanzibar na Wakala wa Majengo hazikuwepo wakati wa uandaaji wa bajeti lakini taasisi husika zinaendelea na majukumu yake kupitia watendaji wake, Wizara ililazimika kupitisha bajeti ya taasisi hizo ili ziweze kutekeleza majukumu yake. Aidha, utaratibu wa kuundwa Bodi hizo umeshaanza kwa Mheshimiwa Rais kuteua Wenyeviti na utaratibu wa kupata wajumbe unaendelea.	Kwa kuwa katika utekelezaji wa majukumu ya Bodi ya Usajili ya Wakandarasi Zanzibar na Wakala wa Majengo unategemea uwepo wa Bodi za Wakurugenzi. Kamati inaishauri Serikali kuwa na usimamizi wa karibu wa utendaji wa bodi pamoja na kufahamu muda wa kumaliza kwake ili ziweze kuundwa upya pale zinapomaliza muda wake. Hatua hii itasaidia kuepusha uvunjaji wa sheria zinazounda taasisi hizi ambazo zinaelekeza bajeti kupitia katika Bodi za Wakurugenzi kabla kufikishwa katika ngazi ya Wizara.

AFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ			
SNo.	HOJA ZILIZOIBUKA	MAJIBU YA WIZARA	MAONI YA KAMATI
1.	Katika makadirio ya mapato na matumizi ya Afisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2023/2024, hakukutolewa taarifa ya utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Masoko ya Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini ambao uliidhinishwa kupitia bajeti ya ziada (supplementary budget). Kamati inaomba kupatiwa uchambuzi wa utekelezaji wa mradi huo.	Jumla ya gharama ya Mradi wa Ujenzi wa Masoko ya Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini ni TZS 69.773 bilioni ambapo jumla ya TZS 33.233 bilioni zimeshapatikana sawa na asilimia 47.6 ya makadirio. Hivyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya TZS 36.539 bilioni zitahitajika kumalizia ujenzi wa masoko hayo kwa mujibu wa mikataba iliyopo.	Pamoja na Kamati kupokea majibu iliyopatiwa katika hoja hii, Kamati inaishauri Afisi ya Rais - Fedha na Mipango kuzipatia fedha taasisi husika ili ziweze kutekeleza miradi yake yenyewe badala ya kuendelea na utaratibu wa baadhi ya fedha za miradi kubakia Afisi ya Rais - Fedha na Mipango.

MAENEO AMBAYO YALICHANGIWA NA WAJUMBE WENGI

Mheshimiwa Spika, Wakati wa mjadala wa Bajeti, baadhi ya maeneo yalichangiwa na Wajumbe wengi zaidi na baadhi ya maeneo hayo yalichangiwa kwa hisia na msisitizo mkubwa. Kwa lengo la kuikumbusha Serikali ili kuichukulia michango hii kwa uzito maalum na kwa kuwa hii ni hotuba ya majumuisho Kamati yangu imeona ni vyema kuchukua fursa hii kuyataja maeneo hayo japo kwa uchache wake ili Serikali iweze kuyafanyia kazi kwa weledi na kwa haraka iwezekavyo. Maeneo haya ni kama yafuatayo:

Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais – Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi

Mheshimiwa Spika, Katika mjadala wa bajeti ya Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Wajumbe wengi walichangia kwa msisitizo suala Muundo wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi, maslahi ya watendaji Pamoja na upatikanaji wa gari kwa ajili ya kazi za Kamati. Aidha, suala la ujenzi wa Afisi za Baraza pia limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wajumbe. Kamati inaungana na Wajumbe kuisisitiza Serikali kutekeleza masuala haya kama ilivyoahidi wakati wa kupitisha bajeti hii. Aidha, Kamati inaikumbusha Serikali kwamba iliahidi kuchukua hatua kwa baadhi ya changamoto hizo kabla ya mkutano huu wa bajeti kumalizika.

Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wengi wamezungumzia uhaba wa watendaji katika Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ambayo ina upungufu mkubwa wa watendaji. Kwa sasa Mamlaka ina watendaji 38 tu wakati mahitaji ni watendaji 118. Kamati inaishauri Serikali kulitafutia ufumbuzi wa haraka suala hili ili kuiwezesha Mamlaka kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ili iweze kupambana na janga la dawa za kulevya ambalo linaiathiri jamii yetu.

Afisi ya Rais - Kazi Uchumi na Uwekezaji

Mheshimiwa Spika, Suala la kuwasimamia na kuwafuatilia wawekezaji nchini limesisitizwa sana na Wajumbe walipokuwa wakichangia Afisi hii ya Rais. Serikali inapaswa kujiridhisha kwamba wawekezezaji wanafuata taratibu zote za uwekezaji zilizoekwa ili nchi yetu iweze kunufaika katika uwekezaji unaofanyika.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wengi wameweka msisitizo mkubwa katika stahiki za walimu kutokulipwa kwa wakati ikiwemo fedha za kusimamia mitihani ya darasa la saba na kidato cha pili, fedha za likizo, nauli na pia posho zinazolipwa kwa walimu wakuu na wasaidizi kwa kiwango cha elfu thalathini ni ndogo sana. Hivyo, Kamati inaitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuhakikisha inasimamia vyema malipo ya stahiki za walimu sambamba na kuweka mpango mahsusi wa kuhakikisha kuwa, walimu wanaendelea kupatiwa stahiki zao kwa wakati ili waendelee kutekeleza majukumu yao kwa morali nzuri na kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Jambo jengine ambalo limesisitizwa ni umuhimu wa vyuo vya ualimu nchini ambavyo hutoa misingi iliyo bora juu ya mbinu za kufundishia kama ilivyokuwa katika chuo cha ualimu Nkurumah. Kuwepo kwa vyuo hivi kunasaidia sana kupata walimu wenye sifa stahiki kwani katika kipindi hiki kumekuwepo baadhi ya walimu wanaokosa mbinu za kufundishia hali inayoathiri kiwango cha elimu nchini.

Afisi ya Rais - Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zina mchango mkubwa katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali ingawaje Wajumbe wengi wamechangia juu ya kushuka kwa mapato yanayokusanywa na Mamlaka hizo kutokana na baadhi ya Wizara na taasisi zinazohusika katika ukusanyaji wa mapato hayo kutokufanya marejesho kwa wakati. Kamati inazitaka Wizara na taasisi hizo zinazohusika na kufanya makusanyo kuhakikisha zinafanya marejesho kwa wakati ili kuongeza ufanisi na kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na kuweza kutekeleza majukumu yaliyopangwa kwa wakati.

Wizara ya Kilimo Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo

Mheshimiwa Spika, Eneo jengine ambalo Wajumbe walichangia kwa msisitizo ni kuimarishwa kwa miundombinu ya umwagiliaji kwa maeneo ya Unguja na Pemba ili kuongeza uzalishaji wa mazao mbali mbali. Aidha, Wajumbe walisisitiza Wizara ya

Kilimo Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, kuweka mikakati na mipango madhubuti ambayo itasaidia katika kuimarisha uzalishaji wa zao la nazi ambalo kwa sasa upatikaji wake ni wa kiwango kidogo hali iliyochangia kupanda bei kwa zao hilo.

Mheshimiwa Spika, Suala la upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima nalo limechangiwa na Wajumbe wengi. Licha ya Serikali kutoweza kutoa pembejeo hizo bure kwa wakulima hao, bado Kamati inaweka msisitizo wa kuitaka Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji na Mifugo kuendelea kutoa elimu na mbinu bora kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji.

Wizara ya Afya

Mheshimiwa Spika, Katika Wizara ya Afya Wajumbe wengi walichangia suala la upungufu wa vifaa tiba katika wodi ambayo inatumika kuhifadhia watoto waliozaliwa kabla ya muda (watoto njiti) hali inayopelekea kuhatarisha maisha ya watoto hao. Kamati inaisisitiza Wizara kuchukua juhudi za haraka juu ya upatikanaji wa vifaa hivyo kwa kuzingatia mahitaji halisi za wodi hizo ili kuokoa maisha ya watoto hao.

Mheshimiwa Spika, Eneo jengine lililochangiwa na Wajumbe wengi katika Wizara hii ni ongezeko la idadi ya vifo vya mama na mtoto licha ya Wizara kupitia watendaji wake kuwapatia elimu ya afya ya uzazi kwa mama hao. Katika kupunguza idadi hii, Kamati inaisisitiza Wizara kuendelea kutoa elimu ya afya kwa mama wajawazito, kuchukua hatua mbali mbali za kuimarisha afya ya mama na mtoto pamoja na kuendelea kuchukua hatua za kinidhamu kwa watendaji wa sekta ya afya watakaobainika kutekeleza majukumu yao kinyume na utaratibu uliopangwa.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

Mheshimiwa Spika, Wajumbe pia walichangia kuhusiana na kuliimarisha Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) kiutendaji. Kamati inaunga mkono hoja hii na kusisitiza katika suala la kuboresha vipindi vinavyorushwa hewani viwe vyenye kuelimisha jamii ili kuongeza idadi ya watazamaji wanaofuatilia vipindi hivyo pamoja na kuliingizia Shirika hilo mapato hasa kwa kuzingatia ushindani mkubwa wa kibiashara uliopo katika tasnia ya Habari kwa sasa. Aidha, Kamati inaipongeza ZBC kwa hatua za hivi karibuni za kuimarisha vipindi vyake.

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale

Mheshimiwa Spika, Michango ya Wajumbe wengi katika Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ilisisitiza juu ya suala zima la uimarishaji wa maeneo ya kihistoria yaliyopo katika kisiwa cha Pemba kwa kuzingatia kwamba maeneo hayo ni muhimu katika kukuza utalii nchini na kuingizia mapato Serikali. Kamati inakubaliana na hoja hii na kuitaka Serikali kulisimamia vyema jambo hili na kuhakikisha kuwa maeneo ya vivutio yanatunzwa na kuimarishwa kwa faida ya vizazi vya sasa na baadae.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto

Mheshimiwa Spika, Katika Wizara hii, miongoni mwa mambo yaliyozungumzwa kwa msisitizo na kwa hisia kubwa ni kuendelea kuwepo kwa vitendo vya udhalilishaji katika nchi yetu. Kamati inainasihi Serikali na wananchi kwa ujumla kuendelea na juhudi za kupambana na vitendo hivi thakili kwani vinaleta haiba mbaya kwa nchi yetu na mustakabali wa vizazi vyetu.

Mheshimiwa Spika, Eneo jengine ambalo Wajumbe walilichangia ni kuchelewa kuwasajili baadhi ya wazee wanaostahiki kupata pencheni jamii. Kamati inaisisitiza Serikali kuchukua hatua za haraka ili kila mzee anayestahiki apate haki yake na kusiwepo malalamiko haya. Kunaweza kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa taarifa za wazee hao lakini changamoto hii inaweza kutatuka kwa kuwekwa mfumo mzuri wa ukusanyaji wa taarifa hizo, mathalan kunaweza kuwekwa namba maalum ya simu kwa ajili ya kukusanya taarifa na malalamiko ya wazee wanaostahiki kupata Pencheni Jamii.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi

Mheshimiwa Spika, Suala la Serikali kuongeza umakini katika mchakato wa ununuzi wa boti mbili mpya za mwendo kasi ni jambo lililosisitizwa sana na Wajumbe waliopata fursa ya kuchangia katika Wizara hii. Kamati inaunga mkono msisitizo huu uliowekwa na Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu itasaidia kuongeza ufanisi wa uendeshaji wa Shirika la Meli na pia itasaidia kuepusha hasara ya kugharamia matengenezo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Eneo jengine ambalo Wajumbe walilichangia kwa msisitizo ni kuwepo kwa changamoto ya uchelewaji wa malipo ya fidia kwa wananchi ambao makaazi na vipando vyao huathirika wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Jambo hili linapaswa kufanyiwa kazi kwa haraka kwani linawarudisha nyuma sana wananchi kimaendeleo. Kamati inainasihi Serikali, pale wananchi wanapomaliza kufanyiwa tathmini ya majengo au vipando vyao kuwalipa haraka fidia zao vyenginevyo italeta athari kubwa kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Suala la kuwepo kwa changamoto ya ufanisi mdogo wa uendeshaji katika bandari ya Malindi nalo lilichukuwa muda mkubwa wa Wajumbe kulichangia kwa msisitizo mkubwa. Licha ya Serikali kuchukua hatua mbali mbali ili kutatua changamoto hiyo lakini Wajumbe wengi walisisitiza Serikali kuongeza umakini katika utekelezaji wa hatua hizo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa katika bandari yetu. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuendeleza juhudi hizi za uimarishaji wa Bandari ya Malindi sambamba na kuongeza juhudi ya ujenzi wa bandari ya Mkoani pamoja na ujenzi wa bandari ya Mangapwani. Kukamilika kwa miradi hii itakuwa ni muarubaini wa kudumu wa changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, Suala la barabara nyingi kuwa mbovu na kuchimbuka hasa katika kipindi cha mvua lilichangiwa kwa msisitizo mkubwa na Wajumbe wa Baraza lako. Ili kutatua changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali ianze utaratibu wa kuzijengea mitaro barabara zetu na zile mpya zinazojengwa ihakikishe suala la ujenzi wa mitaro linakuwemo katika makubaliano na wakandarasi. Hii itasaidia barabara zetu kudumu muda mrefu bila ya kuathiriwa na maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na kuwepo kwa vitendo vya uvunjaji wa Sheria ya Usalama Barabarani kwa vyombo vya moto hususan bodaboda, Wajumbe wengi waliweka msisitizo kwa Serikali kuendelea na juhudi za kudhibiti vitendo hivi kwani vinarudisha nyuma hatua za maendeleo. Serikali inatumia fedha nyingi katika ununuzi wa dawa na pia tunazibebesha hospitali zetu mzigo mkubwa kuwahudia majeruhi wa ajali za barabara. Aidha, Kamati inachukua nafasi hii kuwanasihisi wananchi kujiepusha na vitendo hivi kwani itasaidia kwa kiasi kikubwa kuokoa maisha na mali.

Mheshimiwa Spika, Jambo jengine ambalo limesisitizwa sana katika Mkutano huu

wa Bajeti ni kuwepo kwa changamoto ya usafiri kwa njia ya bahari kati ya Unguja, Pemba na Tanga. Kamati inaridhika na juhudi za Serikali katika kutatua changamoto hii lakini inaitanabahisha iongeze juhudi kwani usafiri wa uhakika baina ya maeneo hayo utakuwa kichocheo kikubwa cha kuimarisha biashara katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba na kupelekea kuinua uchumi kwa wajasiriamali na nchi yetu kwa ujumla.

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi

Mheshimiwa Spika, Kuendelea kuwepo kwa migogoro ya ardhi na kuchelewa kwa kesi za migogoro hiyo katika mahkama ni miongoni mwa maeneo yaliyojadiliwa na Wajumbe wengi tena kwa msisitizo mkubwa. Kamati inaishauri Serikali, iongeze kasi katika zoezi la utambuzi wa ardhi. Hatua hii itasaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa migogoro ya ardhi na hatimae kuipunguzia mahkama ya ardhi mzigo mkubwa wa kuwepo kwa utitiri wa kesi zinazotokana na migogoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, Jambo jengine ambalo limesisitizwa sana ni kuwepo kwa hali ya uchakavu katika nyumba za maendeleo. Serikali kupitia Shirika la Nyumba inapaswa kuendelea kufanya ukarabati kwa baadhi ya nyumba na nyumba nyengine zijengwe upya. Ili kufikia hatua hiyo, Kamati inaishauri Serikali kulisaidia Shirika kuhakikisha inakusanya mapato yake kwa ufanisi. Wapangaji wengi wa nyumba za Shirika hawalipi kodi hali ambayo inaathiri kwa kiasi kikubwa ukusanyaji wa mapato ya Shirika na kupelekea kushindwa kufanya ukarabati wa nyumba zake au kutekeleza miradi ya maendeleo.

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi

Mheshimiwa Spika, Katika Wizara hii michango ya Wajumbe wengi ilijielekeza katika changamoto ya ZAFICO kushindwa kuziendesha meli za SEHEWA zilizonunuliwa. Licha ya Serikali kupanga kuingia mikataba na kampuni binafsi kuhusu uendeshaji wa meli hizo. Hofu ya Wajumbe ni kwamba umefanyika ununuzi wa meli za uvuvi bila ya kuwepo mikakati ya namna uendeshaji wake utakavyokuwa. Meli zimenunuliwa lakini ni muda mrefu hazijatumika. Kamati inashauri, kabla ya kuchukuliwa hatua yoyote ni lazima Serikali au taasisi ya umma iwe imeshaweka mikakati madhubuti ya namna ya kutekeleza shughuli iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kuchelewa kwa utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa bandari za uvuvi ni eneo jengine ambalo limechangiwa sana na Wajumbe. Kumekuwepo na hatua mbalimbali za Serikali kutekeleza miradi hii. Kamati inaisisitiza Serikali wakati huu wa kutekeleza hatua za awali za miradi kama vile kutafuta wakandarasi au kuingia mikataba na wabia, kuongeza umakini katika utekelezaji wake ili hatua hizo ziende kwa haraka bila ya kurudi nyuma.

Wizara ya Maji, Nishati na Madini

Mheshimiwa Spika, Katika Wizara hii Wajumbe waliisitiza Serikali kuendelea na juhudi za kuhakikisha upatikanaji wa maji katika maeneo yetu unakuwa wa uhakika. Ingawa Serikali imechukua hatua mbali mbali kutatua changamoto hii kama vile kujenga matangi ya kuhifadhia maji na kuchimba visima, kuna umuhimu mkubwa pia kuelekeza nguvu katika kutengeneza miundombinu ya mtandao wa maji ili kuweza kufika katika maeneo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wengi pia waliweka msisitizo mkubwa walipokuwa wakichangia Wizara hii kwa kulitaka Shirika la Umeme kutafuta ufumbuzi wa haraka wa changamoto ya kuzima kwa umeme mara kwa mara katika baadhi ya maeneo hususan maeneo ya Fuoni. Kamati inaungana na Wajumbe kuweka msisitizo katika suala hili la umeme kwani upatikanaji wa umeme wa uhakika ni jambo muhimu sana si kwa shughuli za kijamii tu bali hata kwa shughuli za kiuchumi.

Afisi ya Rais - Fedha na Mipango

Mheshimiwa Spika, Katika Afisi hii ya Rais, suala la kutengwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Serikali ni jambo lililositisitizwa sana. Wajumbe wameisisitiza Afisi ya Rais - Fedha na Mipango kuhakikisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Serikali zinagaiwa kwa taasisi husika ili utekelezaji uweze kufanyika, hii ni kutokana na kwamba hii ni bajeti ya tatu inayoainisha fedha hizi lakini hakuna utekelezaji uliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, Eneo jengine ambalo Kamati yangu inaisisitiza Serikali kulifanyia kazi kwa haraka iwezekanavyo ni kuinganisha mifumo yote ya ukusanyaji mapato katika mfumo mkuu wa mapato. Ili kufikia lengo la kukusanya mapato kwa ufanisi

sambamba na kudhibiti mianya ya uvujaji mapato hayo, Kamati inaisisitiza Serikali kuiwezesha mifumo yote ya ukusanyaji wa mapato kusomana na kuiunganisha katika mfumo mkuu wa mapato. Hatua hii itasaidia kuonesha kwa uwazi mapato yanayoingia kwa kila chanzo na eneo husika.

HOJA ZA JUMLA

Mheshimiwa Spika, Katika mjadala wa Bajeti, mbali ya hoja za kibajeti zilizoibuka na hoja zilizochangiwa na Wajumbe wengi, zipo pia hoja za jumla ambazo zimejitokeza katika Wizara zaidi ya moja. Hivyo, Kamati imeona ni muhimu kuyasisitiza maeneo hayo na kutoa maoni na ushauri wake kwa Serikali ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Miongoni mwa hoja hizo ni pamoja na uchakavu wa baadhi ya majengo ya skuli na ofisi za Serikali ikiwemo majengo ya mahkama. Kamati inaitaka Serikali kusimamia suali hili na kuhakikisha kuwa maeneo yaliyo chakavu yanaimarishwa kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Suala jengine ni kuwepo kwa upungufu wa bajeti kwa Wizara na taasisi nyingi za Serikali ambayo inakwamisha ufanisi katika utekelezaji wa majumuku ya taasisi hizo. Hivyo, Serikali inapaswa kupanga bajeti inayotekelezeka na kuhakikisha kila taasisi inapata mgao wa fedha ambao utawawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kiwango kinachostahiki.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande mwengine, Kamati inaisisitiza Serikali suala la kuwawezesha watendaji katika kujiongezea elimu na maarifa kwa kada wanazozitumikia. Jambo hili linahitaji mashirikiano na Wizara husika katika kuhakikisha kuna mpango maalum unaofahamika Serikalini wa kuwawezesha watendaji kupata fursa za kujiongezea elimu na ujuzi kwa maeneo wanayoyafanyia kazi. Kufanya hivi kutapunguza kuondoa changamoto iliyopo kwa baadhi ya taasisi kukosa wataalamu wa kutosha katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Jambo la mwisho ambalo Kamati ya Bajeti imeliona ilisisitize kutokana na umuhimu wake kwa maendeleo ya nchi yetu ni kuwepo kwa utekelezaji mdogo au kutotekelezwa kabisa kwa miradi ya maendeleo. Hali hii ya kuwepo miradi

mingi katika bajeti zetu bila ya kutekelezwa ni dalili kwamba bajeti zetu hazina uhalisia. Tunapanga mambo mengi lakini tunatekeleza machache tena bila ya kukamilika. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kwa mara nyengine tena, kupanga bajeti ambazo tutaweza kuzitekeleza kwa asilimia kubwa. Vile vile, Serikali iongeze juhudi katika usimamizi wa fedha za miradi ya maendeleo ili kuepusha fedha hizo kutumika kinyume na malengo yaliyokusudiwa.

HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Kwa kumalizia napenda kukushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha Hotuba hii ya Kamati ya Bajeti kuhusu Majumuisho ya Mjadala wa Makadirio ya Bajeti kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Kwa upekee nawashukuru pia Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza, Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wengine wa Serikali walioitikia wito wa Kamati kwa kuja katika vikao na kuipa mashirikiano makubwa Kamati ya Bajeti yaliyowezesha Kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Mwisho kabisa, naomba niwashukuru tena Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kuwa watulivu na kunisikiliza kwa umakini wakati nikiwasilisha Hotuba hii ya Kamati ya Bajeti kuhusu Majumuisho ya Mjadala wa Makadirio ya Bajeti kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Ahsante,

.....

Mhe. Abdulla Hussein Kombo,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.